**NAMBA 1: MARKO 1:1-20. UTANGULIZI NA KUITWA KWA WANAFUNZI WA KWANZA:**

Tangu nimepokuwa hapa nchini Tanzania, nikiifanya kazi na Taasisi ya Biblia na Utumishi, nimefundisha masomo **manne** tofauti. Mnamo mwaka **elfu mbili na kumi na nne**, niliwafundisha kutoka Kitabu kinachoitwa "*Miraculous Movements"* - *"Harakati za Kimiujiza".* Tuliangalia kile ambacho Mungu anakifanya miongoni mwa Waislamu katika Afrika. Mnamo mwaka **elfu mbili na kumi na tano**, nilifundisha juu ya Roho Mtakatifu. Yeye ni nani, jinsi alivyo, kile alichokifanya katika Agano la Kale na Agano Jipya, na kile anachokifanya katika maisha ya muumini. Mnamo mwaka **elfu mbili na kumi na saba** tuliangalia suala la uongozi. Nasi tulikitumia kitabu na Askofu Donald Mtetemela, kinachoitwa, "*Show me a leader with Moral Integrity*" - *"Nionyeshe Kiongozi Mwadilifu"*.

Katika mwaka **elfu mbili na kumi na nane**, tulijifunza Barua ya Kwanza ya **Petro**. Na baadaye, kama unataka, unaweza kununua kitabu, nilichoandika kuhusu Barua ya kwanza ya Petro. Bei ni elfu mbili. Mwaka huu utakuwa mwaka wangu wa **tano**, na wa mwisho wa mafundisho, na ninataka kufundisha kutoka kwenye moja ya injili. Nataka tujifunze injili ya **Marko** na tutaangalia juu ya huduma ya Yesu. Sasa, hata kama Injili ya Marko ni injili fupi sana, hatuwezi kujifunza kila kitu katika kitabu hicho. Hatutakuwa na muda wa kuangalia kila sura, au kila habari. Hivyo, nimechagua baadhi ya matukio makuu katika kitabu hicho, na unaweza kuona kwenye ratiba sehemu ambacho tutaifunza.

Katika sehemu hii asubuhi hii, nataka kufanya utangulizi wa Kitabu cha Marko. Na ninataka kuuliza maswali **manne**. Nani? Lini? Wapi? Kwa nini? Marko alikuwa ni nani? Ni lini aliiandika injili hii? Aliiiandika akiwa wapi? Na kwa nini aliiandika injili hii? Hivyo, kabla ya kuanza masomo yetu, tunatakiwa tumjue zaidi mwandishi. Marko ni nani, na alifanya nini? Na jambo la kwanza kusema, ni kwamba Marko hakuwa mmoja wa mitume, lakini pengine alikuwapo hai wakati wa Kristo, kama kijana mdogo. Baadhi ya wasomi wanafikiri kuwa Marko inajitaja mwenyewe, katika habari ya Yesu akisalitiwa katika bustani ya **Gethsemane**, lakini mtu huyo hakutajwa jina lake.

Hebu turejee kwenye kitabu cha **Marko sura ya kumi na nne, mstari wa hamsini na moja**. Mstari unasema hivi: *"Na kijana mmoja alimfuata Yesu, akiwa hajavaa chochote isipokuwa alijitanda nguo ya kitani. Basi walipomshika, alikimbia akiwa uchi, maana aliliacha vazi nyuma".* Injili zingine hazi-kulitaja jambo hili. Mathayo anataja kwamba wanafunzi wote walikimbia wakati Yesu alipokamatwa, lakini Marko tu anamrejelea kijana huyu, ambaye alikimbia bila nguo. Baadhi ya watu wanafikiri huyu alikuwa ni Marko mwenyewe, ambaye alikuwa akiwafuata wanafunzi wakiwa kwenye bustani.

Kwa kweli mara ya kwanza tunasoma habari za Marko ni katika Kitabu cha **Matendo ya Mitume**. Fungua **Matendo sura ya kumi na mbili, mstari wa kumi na mbili.** Katika hatua hii, Mtume Petro alikuwa ametoroka tu kutoka gerezani huko Yerusalemu. Malaika akamwongoza kutoka gerezani, na katika mitaa ya Yerusalemu usiku ule wa manane. Je, Petro alifanya nini? Hivi ndivyo inavyosema: *"yeye alikwenda nyumbani kwa Mariamu, mama wa Yohana, ambaye pia aitwaye Marko, ambapo watu wengi walikuwa wamekusanyika na walikuwa wakiomba".* Kwa hiyo, sasa tunajua kwamba jina la mama yake lilikuwa ni **Mariamu**, na kwamba pia alikuwa na jina lingine, **Yohana**. Yohana Marko. Utabaini kuwa katika mstari huo kulikuwa na watu wengi waliokusanyika kuomba - hivyo ni lazima kuwa chumba kilikuwa ni kikubwa. Kwa kweli walimu wengi wa Biblia wanafikiria kwamba hiki kilikuwa chumba cha juu, ambako Yesu alishere-hekea mlo wa Pasaka, kabla ya kukamatwa kwake. Inaonekana

kuwa wazazi wa Marko walikuwa wakimiliki nyumba kubwa, na ya kwamba Kanisa la Kwanza lilikutana hapo. Hivyo basi, hata kama Marko alikuwa ni kijana mdogo, aliweza kumjua Yesu na wanafunzi wengine.

Ni kitu gani kingine tunachokijua kumhusu Marko? Naam, tunajua kuwa alikuwa na binamu maarufu ambaye alikuwa mmisionari. Tufungue **Wakolosai sura ya nne, mstari wa kumi**. Nami acha nisome kile kinachosemwa hapo. Huyu ni Paulo anayewaandikia Wakolosai. *"Mfungwa wenzangu Aristarko anatuma salamu zake, na  Marko, binamu wa Barnaba".* Paulo yuko gerezani katika hatua hii, na Marko alikuwa pamoja naye kama mfungwa, ingawa hii ilikuwa ni baada ya miaka mingi kama mmisionari. Kwa hiyo, Marko alikuwa binamu wa Barnaba. Je, ni kwa namna gani kazi ya umisionari ya Marko ilianza? Je, tunajua nini kuhusu wakati wake kama mmisionari? Hebu tuangalie  kitabu cha **Matendo ya Mitume sura ya kumi na tatu, mstari wa tano**, kwa sababu mstari huu utatuambia yote juu ya namna kazi ya Marko ilivyoanza. Paulo na Barnaba wanaanza safari yao ya kwanza ya kimisionari, na sehemu ya kwanza kutembelea ilikuwa ni **Salami**, huko **Kipro**. Lakini hebu tambua ni nani alikuwa pamoja nao: *"walilitangaza Neno la Mungu katika masinagogi. Na Yohana alikuwa pamoja nao kama msaidizi wao".*

Inafikiriwa kuwa huyu Yohana Marko, ndiye ambaye alisafiri na akina Paulo na Barnaba kama msaidizi wa kimisionari. Lakini, katika mistari michache tu ijayo, tunajifunza kwamba Marko aliamua kuondoka, na kurudi nyumbani. Angalia **Matendo sura ya kumi na tatu,  mstari wa kumi na tatu**. "*Kutoka Pafo Paulo na wenzake walisafiri kwenda Perga, ambako Yohana aliondoka akawaacha na kurudi Yerusalemu".* Jina lake kamili halikutajwa, lakini inafikiriwa kuwa huyu ni Yohana Marko. Kwa nini Marko aliwaacha? Sisi hatujui. Labda ilikuwa ni kwa sababu ya ugonjwa. Labda alikuwa amepakumbuka nyumbani kwao. Labda alikuwa bado ni kijana mdogo, na alikuwa na hofu ya safari. Labda hakukubaliana na namna ambavyo Paulo alikuwa akihubiri kwa watu wa Mataifa. Hatujui, na Bibilia haituambii. Lakini tunajua kwamba kitendo hiki kilisababisha mabishano makubwa kati ya Paulo na Barnaba baadaye.

Kisha tuangalia **Matendo sura ya kumi na tano, mstari wa thelathini na saba hadi arobaini**. Jambo hili lilitokea miaka michache baadaye. Paulo na Barnaba waliamua kuwa ni vizuri warudi kwa makanisa ambayo walikuwa wameyapanda huko **Asia**. Angalia katika **mstari wa thelathini na saba**: *"Barnaba alitaka kumchukua Yohana, ambaye pia aliitwa Marko, pamoja nao, lakini Paulo hakufikiria kuwa ni busara kumchukua, kwa sababu alikuwa amewaacha huko Pamfilia na hakuendelea nao katika kazi. Basi yalitokea mabishano kati yao kiasi cha kuachana. Barnaba alimchukua Marko na wakasafiri kuelekea Kipro, lakini Paulo alimchagua Sila".* Paulo alimwona Yohana Marko kama ni mtu aliyeshindwa, na hivyo hakutaka kumchukua katika safari nyingine ya umisionari. Paulo akaamua kwenda na **Sila** njia moja, na Barnaba akaenda njia nyingine akiwa na Yohana Marko. Inaonekana kwamba Paulo hakuwa na imani na Marko tena, na alikuwa hana furaha naye kabisa, wakati Barnaba, ambaye alikuwa akihusiana na Marko, alikuwa mvumilivu kwake. Barnaba alikuwa tayari kumpa Marko nafasi ya pili.

Hata hivyo, ni jambo la kushangaza kuona kwamba, miaka **kumi na miwili** baadaye, Paulo alimpa Marko nafasi ya pili. Kwa kweli inaonekana kwamba Marko akawa msaidizi wa Paulo katika huduma yake. Tayari tumeshaona katika **Wakolasai sura ya nne, mstari wa kumi** kwamba Marko alikuwa gerezani pamoja na Paulo huko Roma, kwa hiyo tunajua kwamba walihudumu pamoja. Na wakati mwingine miaka **mitano** baadaye, Paulo anamwandikia **Timotheo** na kumwomba ampeleke Marko. Kwa nini? Paulo anasema "*yeye ni msaada*

*kwangu katika huduma yangu*" (2 Timotheo 4:11). Kwa hivyo, tunajua kwamba Paulo alimsamehe Marko kwa kumwacha, na tunajua kuwa walifanya kazi pamoja katika huduma kwa miaka michache. Hebu nikusomee rejea nyingine moja, ambayo ni ya muhimu, kwa sababu hapa tunaona kwamba Marko pia alifanya kazi pamoja na mtume mwingine. Barua ya Kwanza ya **Petro, sura ya tano, mstari wa kumi na tatu**: Huyu ni Petro akiandika kutoka Roma, na Marko alikuwa pamoja naye gerezani. Je, Petro anasema nini mwishoni mwa barua yake? "*Ninawatumia salamu kutoka kwa mwanangu Marko*". Hiyo haina maana kwamba Marko alikuwa mtoto wa Petro kimwili, lakini ni kwamba alikuwa ni rafiki wa karibu sana. Na walimu wengi wa Biblia wanafikiria kwamba Marko huenda alifanyika mkristo kupitia huduma ya Petro, ndio maana yeye anamwita kuwa ni mwanaye.

Hivyo, yale tunayoyajua kumhusu Marko ni haya. Jina lake lilikuwa ni Yohana Marko, mama yake aliitwa Mariamu. Alikuwa na binamu aitwaye Barnaba. Alikuwa mmisionari. Alikuwa msaidizi wa Paulo. Alikuwa pia msaidizi na rafiki mwema wa Petro. Alitumia muda mwingi kuwa gerezani kwa sababu ya imani yake, naye ndiye aliyeandika injili ya pili - kwa msaada wa Petro. Kwa kweli, walimu wengi wa Biblia wanasema kwamba, hii ni injili ya Petro, lakini iliandikwa na Marko. Petro alimsimulia Marko habari yote, na Marko ndiye aliyeandikia. Baadaye, kwa mujibu wa mapokeo, Marko ndiye alikuwa mwanzilishi wa Kanisa huko **Alexandria** katika nchi ya **Misri**, na kama ni kweli, ina maana kwamba alikuwa mmoja wa watu wa kwanza kuleta Ukristo katika bara la Afrika. Pia inafikiriwa kwamba aliuawa kwa ajili ya imani yake huko Misri, lakini hatujui kama habari hizi ni za uhakika.

Vipi kuhusu swali hili **'kitabu kiliandikwa lini'**? Tena, hatujui kwa uhakika. Mwandishi hakuweka tarehe katika kitabu chake! Lakini watu wengi wanadhani kiliandika katika kati ya ya mwaka **hamsini na tano** na **sitini na tano** baada ya Kristo, ambao ni muda mfupi kabla ya kifo cha Petro - hivyo ni takribani miaka **elfu mbili** iliyopita! **Aliandika kitabu hiki akiwa wapi**? Huenda alikuwa akiwa Roma. Tunajua kutoka katika Agano Jipya kwamba Marko alikuwa gerezani pamoja na Paulo, na pia Petro, katika siku za mwisho za maisha yao. Kwa hiyo, Marko alikuwa na nafasi ya kuzungumza na Petro walipokuwa huko gerezani, naye Marko aliziandika habari kama vile Petro alivyomsimulia juu ya uzoefu wake kama mfuasi wa Yesu.

Hatimaye, **kwa nini kitabu hiki kiliandikwa**? Inaonekana kwamba wakati Marko alipoandika injili yake, hapakuwa na mtu ambaye alikuwa ameandika historia ya maisha ya Yesu. Kwa hiyo Marko aliamua kuandika akitaka kuweka habari zote za Yesu katika kitabu. Angalia katika **mstari wa kwanza wa sura ya kwanza**: "*Mwanzo wa injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu".* Alitaka kusimulia habari ya Kristo. Na inafikiriwa kuwa aliandika kitabu chake kwa ajili ya Kanisa la Roma – au kwa Wakristo wengine wa Mataifa nchini Italia. Labda alitaka kuwatia moyo Wakristo katika Roma wakati huo, kwa sababu wengi wao walikuwa wakiteswa kwa sababu ya imani yao chini ya mfalme Nero. Alitaka kuwatia moyo kwa kuwakumbusha kwamba Yesu aliyajua yote kuhusiana na mateso. Unaposoma injili hii, utaona kwamba Marko anamwonyesha Yesu kama mtumishi wa mateso.

Utajua pia kwamba injili ya Marko ni injili fupi zaidi katika Agano Jipya, lakini ingawa ni injili fupi zaidi, kuna miujiza zaidi iliyoandikwa ndani yake, kuliko katika injili zingine. Pia ni kitabu rahisi sana - si kigumu, lakini ni kitabu chenye kusisimua sana. Kuna matendo mengi katika injili ya Marko. Kinaonyesha jinsi Yesu alivyofanya mambo mengi. Na unaweza pia kuona kwamba Marko ana neno moja analolipenda. Ni neno '*mara moja au ghafla*'. Kwa mfano: wakati Yesu alipomponya mtu aliyekuwa na ukoma katika **sura ya kwanza** tunaambiwa:

"*mara moja ukoma akamtoka*". Wakati binti wa **Yairo** alipofufuliwa katika **sura ya tano** tunaambiwa kuwa: "*mara msichana akasimama na kutembea*". Neno hili linatumiwa na Marko mara **arobaini na saba**! Katika Luka neno hili limetumika mara **moja** tu, na katika Mathayo mara **saba** tu. Marko anawataka watu kuona kwamba Yesu alitenda mambo kwa haraka, katika hali ya uharaka. Ni injili ya matendo, ambapo mambo hufanyika kwa haraka.

Utaona pia Marko hakuandika habari za kuzaliwa kwa Yesu. Hakuna orodha ya majina ya familia au ukoo wake. Hakuna taarifa yoyote kuhusu maisha yake ya utoto, au akiwa kijana. Kitabu kinashughulika na miaka **tatu** tu ya huduma katika maisha ya Yesu, kikianza na Yohana Mbatizaji. Marko hatuambii mengi kuhusu ubatizo wa Yesu, au majaribu ya Yesu; ni mistari tano tu katika **sura ya kwanza**. Jambo moja la mwisho kuhusu Kitabu cha Marko. Ilikuwa ni injili ya kwanza kuandikwa, na waalimu wengi wa Biblia wanafikiri kwamba Mathayo na Luka waliitumia injili ya Marko, ili iwasaidie katika kuandika injili zao wenyewe. Walinakili sehemu za injili ya Marko, na ndiyo sababu baadhi ya sehemu katika Mathayo na Luka zinafanana. Huo ndio utangulizi wa injili ya Marko. Hebu nizungumzie kidogo juu ya ufuasi, na nini maana ya kuwa mfuasi wa Yesu. Hebu tusome **Marko sura ya kwanza, mstari wa kumi na nne hadi ishirini**.

Kuitwa kwa wanafunzi wa kwanza. Yesu alisema *'Njoo Nifuate'*. Na tunajua kwamba Yesu alisema kitu kile kile kwa Mathayo mtoza ushuru katika **sura ya pili.** '*Njoo unifuate*'. Na Mathayo pia alikuwa mtiifu kwa agizo hilo. Ina maana gani kuwa mfuasi wa Kristo? Inamaanisha nini kuwa mtu anayemfuata Yesu? Unafikiria nini unaposikia neno '*mfuasi* '? Ni neno ambalo Wakristo hulitumia sana, lakini huwa tunamaanisha nini tunapolitumia? Mimi nimetoa orodha ya ufafanuzi ya aina **saba** juu ya maana ya mwanafunzi ni nani.

1. **Namba moja**: Mwanafunzi ni **mfuasi** wa Yesu – mtu ambaye ameitwa na Mungu na ni mwanafunzi aliyejitoa kwa Yesu. Mwanafunzi ni mtu ambaye anataka kujifunza na kufuata. Na tunaona katika **mstari wa kumi na nane** unasema kwamba Simoni Petro na Andrea waliziacha nyavu zao na kumfuata Yesu. Mara moja, waliziacha nyavu zao. Na wala hawakurudi nyuma. Hawakukata tamaa. Walikaa na Yesu kwa miaka **mitatu** na waliendelea kumfuata Yesu.

2. **Namba mbili**: Mwanafunzi ni mtu ambaye ni **mtiifu** kwa Neno la Mungu. Katika **Luka sura ya tano, mstari wa nne** kuna habari kuhusu muujiza wa kuvua samaki: Mstari unasema hivi: *"Hata Yesu alipomaliza kusema alimwambia Simoni Petro; tweka mpaka kilindini mkashushe nyavu mkavue samaki"*. Je, Petro alisema nini? Je, alisema hapana? Alisema hivi: *"kwa sababu ya neno lako nitazishusha nyavu".* Alimtii Yesu, ingawa ilionekana kuwa ni jambo lisilo na maana kwake! Mfuasi wa Yesu ni mtu ambaye ni mtiifu kwa Neno la Mungu: Je, una utii kwa Kristo katika maisha na huduma yako?

3. **Namba tatu**: Mwanafunzi ni mtu ambaye **anajikana mwenyewe**. Katika **Luka sura ya kumi na nne, mstari wa ishirini na saba** Yesu aliwaambia haya wanafunzi: *"mtu yeyote ambaye hataubeba msalaba wake, na kunifuata, hawezi kuwa mwanafunzi wangu".* Hiyo ina maana gani? Je, tunapaswa kubeba misalaba juu ya migongo yetu? Kwa kweli, hapana. Msalaba ilikuwa ni ishara ya kifo. Wakati Yesu alipokufa msalabani alijitoa kabisa – alikuwa tayari kuteseka. Alikuwa radhi kusema '*hapana*' kwa kile alichokitaka, na kusema ‘*ndiyo*’ kwa kile Mungu alichotaka. Alijikana mwenyewe. Mwanafunzi wa Kristo ni mtu anayejikana mwenyewe, huteseka kwa ajili ya injili ikiwa ni lazima, na huendelea kumfuata Yesu hata katika matatizo.

4. **Namba nne**: Mwanafunzi ni mtu ambaye **anawapenda** kaka na dada zake katika Kristo. **Yohana sura ya kumi na tatu, mstari wa thelathini na tano** inasema: *"watu wote watajua kuwa ninyi ni wanafunzi wangu kama mtapendana ninyi kwa ninyi".* Na tunajua kuwa jambo hili ni gumu kulifanya. Tunahitaji kuomba msaada wa Mungu ili atuwezeshe kufanya hivyo. Si rahisi, au sivyo? Baba, tusaidie kuwapenda kaka na dada zetu katika Kristo.

5. **Namba tano**: Mwanafunzi ni mtu yule **anayekua** katika Kristo na **kuzaa** matunda. Kama ukiangalia katika **Yohana sura ya kumi na tano, mstari wa nane** Yesu anatuambia hivi: "*ni kwa utukufu wa Baba yangu kwamba mnazaa matunda mengi, na kuonyesha kuwa ninyi ni wanafunzi wangu".* Baadhi ya watu wanadai kuwa ni wakristo, lakini hawana matunda yoyote. Wao ni kama miti ya maembe isiyo na matunda ya maembe! Je, wewe unakua ndani ya Kristo? Je, unazaa matunda? Je, unaendelea kuwa kama Yesu maishani mwako?

6. **Namba sita**: Mwanafunzi wa Yesu ni mtu ambaye humweka Mungu katika **kiini** ya maisha yake. Mungu anatakiwa kuwa ni wa kwanza katika kila kitu. Katika **Luka sura ya kumi na nne, mstari wa ishirini na sita** Yesu anazungumzia kuhusu gharama ya kuwa mwanafunzi. Anasema: *"kama mtu yeyote akija kwangu naye hamchukii Baba yake, na mama yake, mke wake na watoto wake, ndugu zake waume au wake - naam, hata maisha yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu".* Haya ni mafundisho magumu, au sio? Je, tunapaswa kuchukia familia zetu kwa kweli? Je unafikiri nini? Kuna vifungu vingine katika Biblia ambavyo vinaonekana kusema kinyume chake. Acha nisome kitabu cha **Kutoka sura ya ishirini, mstari wa kumi na mbili** – tunaambiwa hivi: "*Waheshimu baba yako na mama yako*", lakini katika **Luka sura ya kumi na nne** Yesu anasema *"mtu yeyote akija kwangu na hamchukii Baba yake na mama yake, hawezi kuwa mfuasi wa yangu*". Inaonekana kama inasema jambo lililo kinyume.

7. Huu hapa mfano mwingine. **Waefeso sura ya tano, mstari wa ishirini na tano** – Paulo anasema: *"Enyi waume wapendeni wake zenu kama Kristo alivyolipenda Kanisa",* lakini hapa katika **Luka sura ya kumi na nne** Yesu anasema: "*kama mtu yeyote akija kwangu naye hamchukii mke wake*" - hivi ni kweli? Je, maana yake nini jambo hii? Je, ni kweli Yesu anamaanisha nini anaposema kuhusu kuzichukia familia zetu? Anamaanisha haya: mahusiano mengine yote lazima yawe ya pili, baada ya uhusiano wetu na Yesu. Anasema hivi, huwezi kuwa mwanafunzi wangu isipokuwa kama umenipenda mimi zaidi ya vile unavyoipenda familia yako. Hivyo – bila shaka unapaswa kuipenda familia yako – lakini upendo wako kwa Yesu unapaswa kuwa mkubwa zaidi. Mwanafunzi ni mtu ambaye humfanya Yesu kuwa kitu muhimu zaidi katika maisha yake.

8. Na hatimaye, **namba saba**: Mwanafunzi pia ni mtu ambaye anajihusisha katika kuwafanya wanafunzi wengine, huwashirikisha watu wengine imani yake na kuwasaidia kukua kama Wakristo. **Mathayo sura ya ishirini na nane, mstari wa kumi na tisa**: Yesu anawaambia wanafunzi wake: *"enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza na kuwafundisha kutii kila kitu nilicho-waamuru ninyi".* Je, unasaidia katika kuwafanya wanafunzi? Je, unalitii agizo hili la Kristo? Mstari huu unawahusu wanafunzi, kuwafanya wanafunzi wengine. Hii si kazi ya wainjilisti tu, ni kazi ya wachungaji pia. Kwa kweli, ni kazi ya kila Mkristo. Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika injili, na katika Kitabu cha Matendo ya Mitume. Kila Mkristo anapaswa kusaidia katika kuwafanya wanafunzi? Je, unawaambia wengine habari za Yesu?

9. Hivyo, hapo tumekuwa na ufafanuzi na maelezo ya aina **saba** juu ya maana ya kuwa mwanafunzi wa Yesu. Katika mwanzo wa masomo yetu, ni vizuri kufanya kipimo na tathimini ya afya ya kiroho, tunapoangalia nini maana ya ufuasi. Unapotafakari kuhusu maisha na huduma yako, nakutaka ujiulize maswali haya **saba**: Je, mimi ninamfuata Yesu katika maisha yangu? Je, nimekuwa mtiifu kwa Neno la Mungu? Je, ninajikana mwenyewe na kumweka Yesu kuwa wa kwanza? Je, ninawapenda kaka na dada zangu katika Kristo? Je, ninakua katika imani yangu na kuzaa matunda? Je, ninampenda Yesu zaidi ya familia yangu? Je, ninajihusisha katika kuwaambia watu wengine habari za Yesu? Hizi ni ishara ambazo zinamwonyesha mtu kuwa yeye ni mfuasi wa Yesu.

10. Miaka **elfu mbili** iliyopita katika nchi ya Israeli, Yesu aliwaita wanafunzi wake wa kwanza. Hata sasa, bado Yesu anawaita watu waje kwake mwenyewe. Yeye anawaita watu wamfuate Yeye, na pia anawaita watu kama wewe na mimi, ili kuwasaidia watu wengine kumfuata Kristo. Je, Yesu aliwaambia nini akina Simoni Petro na Andrea? *"Njooni mnifuate, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu*". Je, mwitikio wao ulikuwaje? *"Mara moja, wakaondoka na kuziacha nyavu zao na kumfuata Yesu".* Natumaini kwamba hata sisi tutakuwa watiifu kwa Kristo, na ya kwamba tutachagua kumfuata Yeye kila siku katika maisha yetu. Mungu atututie nguvu tunapochagua kufanya hivi.

-----------------------------------------